# OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA

## *Idara ya Usafi na Mazingira*

# HALI YA UHARIBIFU WA MAZINGIRA KWENYE MAENEO YA FUKWE ZA ZIWA VIKTORIA UNAOSABABISHWA NA SHUGHULI ZA BINADAMU ZA KIUCHUMI NA KIJAMII

**Kenyela F.S**
**Afisa Mazingira wa Manispaa**
**MUSOMA**

**JUNE, 2015**

## Utangulizi

Mazingira ni ghala la kuhifadhi malighafi zote zinazohitajika kuendeleza uhai wa viumbe hai na mfumo-ikolojia. Binadamu ni sehemu ndogo sana ya mazingira. Mahitaji yote ya binadamu hutunzwa ndani ya mazingira. Mazingira yanahusisha maumbile halisi yawazungukayo binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabianchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe, hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana.

Binadamu hawezi kuishi kama mazingira yatakoma kumpatia mahitaji yake kama maji, hewa, mwanga wa jua, chakula, udongo/ardhi, sehemu (space), nishati, na mahitaji mengine. Lakini mazingira yataendelea kustawi vizuri zaidi kama binadamu atakoma kuwa sehemu ya mazingira (Man can not live without the environment but the environment can thrive without man).

Kwa bahati mbaya sana binadamu kama mshirika tu wa mfumo ikolojia katika mazingira amegeuka kuwa mharibifu mkubwa wa mazingira kuliko kiumbe mwingine yeyote. Kwa hakika shughuli za binadamu hususan za kiuchumi ndizo chanzo kikubwa zaidi cha uharibifu wa mazingira. Mojawapo ya matokeo hatarishi ya uharibifu huo ni kupotea kwa uoto wa asili (deforestation), kuongezeka kwa hali ya jangwa (desertification), kuongezeka kwa joto duniani (global warming) kunakosababisha mabadiliko ya tabia nchi (climate change), kupungua kwa bioanuai (loss of biodiversity), kutoweka kwa viumbehai (extinction), kutoboka kwa tabaka la ozone, kuharibika kwa udongo/ardhi (land degradation) na mengine mengi. Binadamu anawanyima haki ya msingi ya kuishi katika mazingira bora viumbe wenzake na hata binadamu wenzake katika vizazi vijavyo (Inter generational Equity).

Tukiangalia mazingira ya maji pekee (aquatic ecosystems), kuna kupungua kwa kiasi kikubwa kwa wingi wa viumbe (population), kupungua kwa bioanuai na kupotea kabisa (extinction) kwa aina nyingi za viumbe wa majini wakiwemo samaki. Moja ya visababishi vikubwa ni uvuvi haramu (kutumia sumu, nyavu haramu na baruti), uchafuzi wa maji, kuongezeka kwa joto, na uharibifu unaotokana na kuharibu mazingira yanazoruhusu samaki kuzaliana, kupata chakula na kujikinga na maadui. Viumbe wengi wa majini wakiwemo samaki huzaliana kandokando ya ziwa au bahari. Uharibifu wowote unaofanyika kandokando ya ziwa au bahari huathiri kwa kiasi kikubwa maisha ya viumbe maji.

Mazingira ya fukwe za Musoma zinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo uchimbaji wa mchanga, ujenzi wa majengo ya kudumu, uvuvi haramu, uchimbaji/ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki na kilimo. Shughuli hizi zinafanyika ndani ya mita 60. Changamoto hizi zinahitaji utatuzi wa haraka wa wa kudumu katika kuhakikisha kuwa tunalinda na kutunza mazingira kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo.

Aidha, ushirikishaji wa wananchi katika kutunza mazingira unatakiwa kupewa kipaumbele cha kwanza ndipo hatua zingine zichukuliwe. Hii ni kwa sababu uharibifu wote unaotokea unafanywa au kusababishwa na shughuli za binadamu. Usimamiaji wa sheria za nchi ni suala la lazima ili kudhibiti tabia ya binadamu ya kutafuta maendeleo na kipato kwa gharama ya kuhatarisha usalama wa mazingira. Bila sheria kusimamiwa ipasavyo, maendeleo endelevu hayatapatikana kamwe.

**Mr. Fikiri S. Kenyela**
Afisa Mazingira wa Manispaa
Musoma

## Shukrani

Kwa dhati kabisa napenda kutambua mchango mkubwa wa Mkurugenzi wa Manispaa Dr. Khalfany B. Haule katika kupambana na uharibifu wa mazingira. Ni mtu imara, makini na mpenda mazingira wa hali ya juu. Jeshi la polisi kituo cha kati Musoma siwezi kuwasahau kwa ushirikianao mkubwa wanaonipa katika kusimamia mazingira hususan pale taarifa za watu wanaoharibu mazingira makusudi.

Sitatenda haki kama sitawataja wafuatao kwa nia ya kutambua mchango wao: Rwechungura T.R.K (Afisa Afya - Mkuu wa Idara ya Usafi na mazingira), Simon Weswa (Afisa Mazingira), Thomas Mayombo na Bearling R. Maugo (Wakaguzi wa mji), Anderson Mmbaga (Afisa maliasili) na Hussein Msambwa (Mdau mpenda mazingira kata ya Makoko).

**Fikiri S. Kenyela**
Afisa Mazingira wa Manispaa
Musoma

# Yaliyomo

Utangulizi ..... 2

Shukrani ..... 4

1.0 Uharibifu wa Mazingira ya Fukwe za Ziwa Viktoria Kutokana na Shughuli za Binadamu ..... 6

1.1 UCHIMBAJI WA MCHANGA NA MAWE KWENYE FUKWE ZA ZIWA ..... 6

1.2 Athari za Kimazingira Zinazosababishwa na Uchimbaji Mchanga, Kilimo, Uchimbaji wa Mabwawa ya kufugia samaki na Ujenzi Kwenye Fukwe ..... 11

1.3 Ujenzi Ndani ya Mita 60 za Eneo la Fukwe ..... 15

1.4 Uchimbaji Wa Mabwawa Ya Kufugia Samaki ..... 17

1.5 Kilimo Kandokando ya Ziwa ..... 18

2.0 Sheria Ya Mazingira Na.20 Ya Mwaka 2004 Inachosema Kuhusiana Na Utunzaji Wa Fukwe Na Miambao ..... 19

2.1 Kanuni za Misingi zilizopo katika sheria ya uhifadhi wa Mazingira ya Mwaka 2004 ..... 20

2.2 Sheria Inachosema Kuhusiana Na Fukwe Za Bahari, Maziwa, Mabwawa Na Mito: ..... 24

2.3 Adhabu Za Kisheria Kwa Waharifu Wa Mazingira ..... 25

2.4 Hatua Zinazochukuliwa Na Halmashauri Ya Manispaa Ya Musoma Katika Kudhibiti Uharibifu Wa Mazingira ..... 26

3.0 Changamoto Zinazokwamisha Utunzaji Na Uhifadhi Wa Mazingira Katika Halmashauri Ya Manispaa Ya Musoma ..... 28

3.1 Utatuzi wa Changamoto ..... 29

4.0 Majukumu Ya Mamlaka Za Serikali Za Mitaa Katika Kusimamia Uhifadhi Wa Mazingira ..... 31

4.1 Kamati Za Kudumu Za Mamlaka Za Serikali Za Mitaa ..... 32

4.2 Kamati za Kudumu za Miji, Kata, Vijiji na Vitongoji ..... 32

4.3 Uteuzi wa Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji ..... 33

4.4 Kazi za Ofisa Msimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji. ..... 33

4.5 Madaraka ya jumla ya Kamati za Usimamizi wa Mazingira za Jiji, Manispaa, Wilaya, Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji: ..... 33

5.0 Hitimisho ..... 34

## 1.0 Uharibifu wa Mazingira ya Fukwe za Ziwa Viktoria Kutokana na Shughuli za Binadamu

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ina jumla ya eneo lenye kilometa za mraba 63 na jumla ya wakazi ni 134,327 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012.

Mji wa Musoma

Shughuli za kiuchumi za wakazi wa Musoma ni pamoja na uvuvi, kilimo, ufugaji biashara na ajira serikalini au sekta binafsi. Aidha watu wa Musoma kama ilivyo miji mingine, wanaendeleza maeneo yao kwa kufanya ujenzi mkubwa na mdogo. Ujenzi pia hufanywa na serikali kuu, serikali za mitaa, makampuni, taasisi za dini na watu binafsi. Ujenzi wa nyumba na miundombinu ya barabara, maji na mawasiliano unafanyika ndani ya Manispaa ya Musoma. Madini yote yanayohitajika kwa ajili ya ujenzi wa aina zote yanapatikana kutoka kwenye mazingira. Uchimbaji/uvunaji wa madini ya ujenzi huambatana na athari nyingi za kimazingira.

### 1.1 UCHIMBAJI WA MCHANGA NA MAWE KWENYE FUKWE ZA ZIWA

Uchimbaji wa mchanga katika fukwe za ziwa unaendelea kwa kasi kubwa ndani ya halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Malori, mikokoteni na visandalusi vyote vinatumika kusafirisha mchanga wa ziwani kwenda maeneo ya ujenzi. Fukwe zinaondolewa uoto wa asili, zinaachwa na mashimo na mifereji isiyo ya asili. Mfumo ikolojia wa ziwa umeharibiwa. Uharibifu huu ni mkubwa hasa katika mitaa ya Nyangw'ena, Nyarigamba, Ziwani na Bukanga katika kata ya Makoko. Uchimbaji wa

mchanga pia unaendelea kwa kasi kubwa katika kata ya Mwisenge na kata zingine zenye fukwe.

Mbali na watu na mashirika binafsi, Kwa bahati mbaya sana taasisi za serikali pia zimetajwa kuwa vinara wa uharibifu huo. Baadhi ya shughuli za serikali zinazotajwa kusababisha uharibifu wa mazingira kwa kuchimba na kutumia mchanga wa ziwani ni pamoja na ujenzi wa Maabara unaoendelea katika kila kata, ujenzi wa madarasa katika shule mbalimbali ikiwemo shule ya msingi Mwisenge na ujenzi wa miundombinu ya maji chini ya MUWASA unaofanywa na kampuni ya SPENCON. Kwa namna yoyote ile kama tuna nia ya kuwa na maendeleo yenye tija na endelevu hatuwezi kuunga mkono maamuzi yanayopelekea uharibifu mkubwa wa mazingira kama huo. Bila viongozi wetu wa serikali na siasa kuwa na uzalendo na mapenzi mema na ya dhati kwa mazingira na kupata weledi wa masuala ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira, hali hiyo ya kufanya maamuzi yanayopelekea kuharibu mazingira itaendelea. Elimu ya mazingira kwa viongozi wetu inahitajika sana katika kuokoa mazingira maana wao ndiyo wanaobeba hatima ya maamuzi mbalimbali yatakayopelekea kutunza au kuharibu mazingira. Aidha usimamizi wa sheria ni budi usiwe maoni na utashi wa mtu au kisiasa. Ni suala la lazima. Hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika hali ya kusikitisha zaidi baadhi ya watu wamejipatia viwanja ndani ya mita 60 za ufukwe na kuweza kufanya ujenzi katika maeneo hayo tengefu kinyume kabisa cha sheria na pasipo kujali.

Aidha, katika siku za hivi karibuni kumekuwepo na mwamko mkubwa wa watu binafsi na vikundi hasa vya vijana kujihusisha na biashara ya ufugaji samaki kwa njia ya mabwawa ya kuchimba. Mabwawa haya kwa sehemu kubwa yamechimbwa kandokando ya ziwa ndani ya mita sitini. Kufuatia hali hiyo, uoto wa asili katika ufukwe umeondolewa na viumbe wa asili wa eneo la fukwe kufukuzwa katika maeneo yao au kufa. Na pia hali hiyo imeondolea watu fursa ya kulifikia ziwa kwa matumizi mengine rafiki kwa mazingira ikizingatiwa ziwa ni la watu wote (public property).

Kilimo cha bustani, mazao ya chakula na biashara ni moja ya shughuli za binadamu zinazozuiliwa kufanyika kando kando ya ziwa kwani zinaweza kusababisha kuondoka kwa uoto wa asili wa ufukweni, kusababisha mmomonyoko wa udongo na kuingiza madawa (kemikali) za kuulia wadudu waharibifu wa mazao na mbolea ndani ya ziwa hali inayosababisha kutia sumu kwenye maji na kuleta madhara kwa viumbe na kwa binadamu.

Kandokando ya ziwa pia zipo shughuli za binadamu zinazoruhusiwa kama vile kuoga, kuogelea, shughuli za uvuvi, kuanika dagaa, kugoa vyombo vya usafiri wa majini kama mitumbwi, boti na ngama na shughuli zingine zitokanazo na mazao ya majini. Hata

hivyo usimamizi wa shughuli hizo ni muhimu ili zifanyike pasipo kuwa chanzo cha kuchafua mazingira. Ipo baadhi ya mialo yetu haina choo hata kimoja na ile yenye choo ina matundu yasiyotosheleza wingi wa watu. Masalan mialo mingi ya Kata ya Makoko haina vyoo kabisa. Wavuvi na wafanyabiashara na watu wanaotembelea mialo hulazimika kujisaidia ovyo haja kubwa na ndogo ndani ya maji, kwenye mchanga au kwenye vichaka vilivyo kandokando ya ziwa. Huu ni uchafuzi mkubwa wa mazingira hali inayohatarisha afya ya wavuvi, wafanyabiashara na watumiaji wote wa maji hayo. Ni wazi kuwa kwa uduni wa teknolojia iliyopo katika kukausha dagaa, wavuvi wetu na wafanyabiashara hukausha dagaa kwa kuwaanika chini kwenye mchanga moja kwa moja bila hata kuweka maturubali. Kwa hali kama hiyo tusishangae kukuta dagaa wameanikwa kwenye kinyesi cha binadamu.

Hatua za haraka ni vyema zikachukuliwa ili kujenga vyoo vya umma katika mialo yetu yote ili kuepusha uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha afya ya watu. Baada ya vyoo kuwepo, ni lazima kuwe na usimamizi wa kuzuia watu kujisaidia ovyo. Matumizi bora ya vyoo yapewe kipaumbele

Uchimbaji mchanga unavyosabaisha uharibifu wa mazingira Makoko-Musoma

Pamoja na kutunza fukwe, ni vizuri tukakumbuka kuwa shughuli zinazofanyika ukanda wa juu zinaweza kusababisha mazara ukanda wa chini. Kwa mfano kilimo kisicho bora kwenye milima licha ya kuharibu mlima wenyewe husababisha pia uharibifu wa maji ziwani ambako udongo utiririshwao na maji ya mvua huishia. Pia utiririshaji wa maji taka/machafu kutoka kwenye viwanda, garage, carwash, nyumba za kuishi, hospitali, magereza, shule na taasisi zingine hatima yake ni kuingia ziwani. Maji machafu hayo yaweza kutiririshwa kupitia mitaro au mito au moja kwa moja kwenye mabomba kuelekea ziwani. Hali hii isipodhibitiwa huleta mazara makubwa kwa viumbe na afya ya binadamu.

Maji machafu/taka yasiingizwe ziwani moja kwa moja pasipo kutibiwa ili kupunguziwa au kuondolewa mazara kabla hayajaingia ziwani.

Hali hii isipodhibitiwa tutalaumiwa na vizazi vijavyo

**Changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana na uharibifu wa mazingira (ajira haramu)**

Vijana wamejiajili katika uharibifu wa mazingira ya fukwe huko Mwisenge – Je hiyo ni ajira halali?

## 1.2 Athari za Kimazingira Zinazosababishwa na Uchimbaji Mchanga, Kilimo, Uchimbaji wa Mabwawa ya kufugia samaki na Ujenzi Kwenye Fukwe

Uchimbaji wa mchanga, kilimo na ujenzi kwenye maeneo ya fukwe husababisha athari kubwa za kumazingira na kijamii kama ifuatavyo;-

Eneo la ufukwe ni mpaka wa makazi (ecotone) kwa makazi (habitat) ya nchi kavu na makazi ya maji kwa ajili ya maisha ya viumbe hai. Kuna aina nyingi sana za viumbe hai ambao wameumbwa kuishi katika mazingira hayo. Viumbe mbalimbali kama aina mbalimbali za reptilia, amphibia, ndege, mammalia, wadudu na samaki hutumia eneo la ufukwe kukidhi mahitaji mbalimbali ya maisha yao kama ifuatavyo:

1. Ndege hutengeneza viota vyao kwenye mimea iliyopo kandokando ya ziwa na kukuza vifaranga vyao pale. Kuharibu mimea ya asili kwenye fukwe huondoa uwezekano wa ndege kuzaliana na kuishi katika mazingira ya asili. Jamii mbalimbali za ndege huishi kando kando ya ziwa pekee. Ndege hao huishi kwenye maeneo ya mpaka wa makazi ya nchi kavu na maji. Ndege hula viumbe

wa majini kama samaki na wadudu. Uharibifu kwenye ufukwe husababisha kuangamia kwa ndege kufuatia kukosa makazi na kushindwa kuzaliana. Ndege huhama, hufa, kushindwa kuzaliana, hupungua idadi (population) na hutoweka kabisa (extinction). Miaka michache tu iliyopita hali ilikuwa tofauti. Mida ya asubuhi ungesikia sauti nyingi za ndege wakiimba kwa sauti mbalimbali na jioni kuimba tena kwa nguvu wanaporejea kutoka mawindoni ili kulala. Ungeona viota vingi vya ndege vikiwa na mayai au vifaranga. Kwa sababu ya uharibifu wa fukwe hali hii haipo tena. Ndege wengi wametoweka na waliosalia idadi yao inapungua kila kukicha.

*Ndege hutumia eneo la ufukwe kama makazi na eneo la kupata chakula na kujidai*

2. Mimea na uoto wa asili hutoa chakula kwa viumbe mbalimbali katika eneo la ufukwe. Majani ya miti, vichaka na vyasi huingia ndani ya maji upepo uvumapo na huweza kuwa chakula kwa viumbe walioko majini. Pia husababisha kukua kwa mimea ya majini ambayo pamoja na kuwa chanzo cha chakula kwa viumbe ndani ya maji, huzalisha hewa ya oksijeni ndani ya maji kupitia photosynthesis, hewa ambayo ni muhimu kwa viumbe. Kuharibu mimea kwenye ufukwe kwa sababu yoyote ile huathiri maisha ya viumbe wa majini.

3. Majani ya mimea huwa ni chakula kwa samaki na viumbe wengine.

4. Viumbe wengi kama kenge, nyoka, mamba n.k hutaga mayai yao kwenye mchanga wa ufukweni. Kuchimba fukwe husababisha viumbe hawa kupoteza mayai yao, kushindwa kutaga na hivyo hushindwa kuzaliana na idadi yao kupungua sana. Samaki nao hukuza vifaranga wao kandokando kabisa mwa ziwa kwenye kina kifupi hadi mahali mawimbi yanapoishia. Uharibifu wa aina yoyote wa ufukwe huleta mazara makubwa kwa samaki hususan uwezo wao wa kuzaliana. Suala hili lina athari za kiuchumi kutokana na ukweli kwamba samaki hawatazaliana na kukua kwa wingi. Pato la mvuvi na taifa kwa ujumla hushusha pamoja na kuikosesha jamii kitoweo na virutubisho vya protein.

5. Viumbe wengi huota jua wakati wa mchana hasa kwenye mchanga, uwazi na mawe/miamba iliyopo kandokando ya ziwa. Kuharibu fukwe nikuwaweka jela viumbe wa asili.
6. Miti inayoanguka ndani ya maji kandokando ya ziwa haipaswi kuondolewa kwani huwa ni sehemu nzuri ya viumbe kujificha, kuota jua na kupata chakula.

Mimea iliyo kandokando ya ziwa ina manufaa makubwa kwa viumbe hata ikianguka majini.

**Samaki hunufaika na mimea iliyo kandokando ya ziwa.**

7. Uoto wa asili kando kando ya ziwa husaidia sana kuzuia mmomonyoko wa udongo ambao ungeingiza udongo usiofaa ndani ya maji na kuharibu kingo za ziwa. Kuwepo kwa uoto huo hufanya kingo za ziwa ziwe salama bila kuharibiwa na mawimbi makali ya ziwa na hivyo ikolojia ya ufukwe na viumbe waliopo hubaki wamelindwa na kuhifadhiwa katika mazingira rafiki.

8. Uharibifu wowote ule wa maeneo ya fukwe husababisha mabadiliko ya maumbile ya asili kwenye eneo hilo na kuathiri maisha ya viumbe hai ikiwemo kufa kwa viumbe, kukimbilia maeneo yasiyo rafiki kwao, na kutoweka kabisa kwa aina za viumbe hao kwenye mazingira yetu (extinction).

   Kutokana na sababu za kuharibu mazingira ya asili ya fukwe za ziwa na bahari viumbe wengi waliokuwepo zamani leo wametoweka kabisa (extinction) wakiwemo samaki, ndege wa aina mbalimbali, reptilia na amphibian, mammalian na wadudu. Kipindi cha nyuma ungesikia sauti nzuri za ndege wengi kila ufikapo ufukweni mida ya asubuhi na jioni lakini leo zimefifia sana na sana na baadhi ya maeneo sauti hizi za ndege zimekoma kabisa. Hiki ni kiashiria kikubwa sana cha uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za kiuchumi za binadamu.

Ona uharibifu ulivyofikia kule Makoko

Aidha kutokana na uchimbaji mchanga na uharibifu wa fukwe za ziwa, maji yamesogea zaidi kwenye maeneo ya makazi ya watu kwa vile maji hufuata mkondo. Kule Makoko, ipo miji ambayo imefikiwa na maji ya ziwa kufuatia uchimbaji holela wa mchanga kwenye fukwe za ziwa.

## 1.3 Ujenzi Ndani ya Mita 60 za Eneo la Fukwe

*Hali iko hivi maeneo mengi hapa Musoma. Kama hali hii ikifumbiwa macho hakutakuwa na fukwe kabisa mda mfupi ujao.*

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, mazingira ya fukwe yameharibiwa sana kutokana na ujenzi wa majengo ndani ya mita 60.

*Uharibifu huu si wa kufumbia macho*

*Ujenzi huu unafanyika kinyume cha sheria za Nchi kwa kusababisha hasara kubwa kwa mfumo ikolojia wa ziwa.*

## 1.4 Uchimbaji Wa Mabwawa Ya Kufugia Samaki

Ni moja ya shughuli za binadamu zinazosababisha uharibifu mkubwa wa mazingira katika fukwe za ziwa viktoria katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. Kama hali hii haitadhibitiwa, mazingira ya fukwe kwa ajili ya viumbe hai yatakuwa yameharibiwa vibaya na kusababisha kupungua kwa bioanuai.

Bwawa la samaki kwenye fukwe za Musoma

Mabwawa ya samaki ufukweni –Musoma, kata ya Kitaji

Shughuli zote hizi za binadamu zilizotajwa hapo juu zinazoendelea kwa kasi kubwa ndani ya eneo la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, licha ya kuwa na lengo zuri la

kukuza kipato na kuinua uchumi, zinasababisha uharibifu mkubwa wa Mazingira. Aidha shughuli hizi za kiuchumi kwa mujibu wa sheria ya Mazingira hazitakiwi kufanyika ndani ya eneo hilo la mita 60 za ufukwe.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma tayari imeshaanza kuchukua hatua za kudhibiti hali hiyo kwa kutoa elimu kwa umma ikiwa ni pamoja na kuwakamata waharibifu wa mazingira kwa

kushirikiana na jeshi la Polisi. Mharibifu wa mazingira atatozwa fain isiyopungua shilingi laki tano (500,000/=). Aidha zoezi la kutoa elimu kwa umma kuhusiana na utunzaji wa Mazingira linaendelea kupewa nafasi kubwa.

## 1.5 Kilimo Kandokando ya Ziwa

Katika fukwe za ziwa viktoria, wapo wakulima wanaofanya shughuli za kilimo cha nafaka na bustani ndani ya mita 60 za eneo la fukwe.

Athari za kilimo kandokando ya ziwa ni nyingi zikiwemo zote ambazo zimetajwa hapo awali zinazosababishwa na uchimbaji wa mchanga na ujenzi kwenye fukwe. Athari zingine ni:

1. Mmomonyoko wa udongo
2. Kuondoka kwa mimea na uoto wa asili kwenye fukwe ambayo ni makazi ya viumbe hai na huchuja uchafu usiingie ziwani kama ulivyo sanjali na kuzuia mmomonyoko wa udongo.

3. Kilimo kandokando ya ziwa husababisha Kumeguka kwa kingo za ziwa na mmomonyoko wa udongo unaosababisha kuua vifaranga vya samaki na kufukia maeneo ya kuzaliana samaki kwenye ardhi chini ya maji.
4. Wakulima hutumia kemikali mbalimbali katika bustani zao ambazo hatahivyo huishia ndani ya maji pindi mvua inaponyesha. Kemikali hizi ni sumu kwa samaki na huchafua maji na kuyafanya yawe na madhara kwa viumbe wengine na hata binadamu.
5. Kuwanyima viumbe hai maeneo yao ya asili ya kujidai.

Athari hizi zitokanazo na kilimo kando ya ziwa ni miongoni mwa visababishi vya kupungua kwa wingi na aina ya samaki katika ziwa viktoria.

## 2.0 Sheria Ya Mazingira Na.20 Ya Mwaka 2004 Inachosema Kuhusiana Na Utunzaji Wa Fukwe Na Miambao

Sheria ya mazingira Tanzania ilitungwa kufuatia kutungwa kwa sera ya taifa ya mazingira mwaka 1997. Sera bila sheria haina nguvu kwani hakuna anayeadhibiwa mahakamani kwa sababu ya kukiuka sera bali kwa kukiuka sheria. Kwa hali hiyo, Sera ya Mazingira ya mwaka 1997 imebainisha wazi (aya ya 70) juu ya umuhimu wa kutungwa kwa sheria itakayosimamia maswala ya mazingira nchini. Vile vile sera hiyo imetaja mambo muhimu ambayo sheria hiyo itayapa kipaumbele nayo ni:-
(a) Upembuzi yakinifu wa athari za mazingira (EIA)
(b) Matumizi ya dhana na viashiria vya kiuchumi
(c) Kuandaa viwango na viashiria vya mazingira (Standards & indicators)
(d) Kutumia kanuni ya kuchukua tahadhari kabla ya athari (Precautionary Principle)
(e) Kuimarisha ushirikiano wa kimataifa

Hivyo uandaaji wa sera na hatimaye rasimu ya sheria ya mazingira ulishirikisha wadau mbalimbali hadi Sheria ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira Namba 20 ya mwaka 2004 ilipopitishwa na Bunge na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais. Ilianza kutumika rasmi tarehe 1 Julai 2005 na kama ilivyotanguliwa kesemwa, Sheria hii imelenga kutekeleza yale yaliyobainishwa ndani ya sera ya mazingira. Kwa vile sheria hii ndiyo sheria mama juu ya uhifadhi wa mazingira nchini na rasilimali zake na inalenga uhifadhi wa mazingira kwa ujumla wake, imeweka misingi thabiti na kanuni za usimamizi endelevu wa mazingira nchini. Vile vile ina ainisha muundo wa kitaasisi wa utunzaji endelevu wa mazingira nchini na kuunganisha mamlaka za taasisi ilikuepuka migongano ikiwa ni pamoja na kuleta ushirikiano wa kiutendaji kati ya wahusika wa idara na wizara mbalimbali.

## 2.1 Kanuni za Misingi zilizopo katika sheria ya uhifadhi wa Mazingira ya Mwaka 2004

Miongoni mwa kanuni hizo ni; **kanuni ya mchafuzi kulipa (Polluter pays principle)**. Sheria hii ya uhifadhi wa Mazingira inatamka wazi kuwa yeyote yule atakayebainika kuchafua mazingira analazimika kulipa kwa kiwango kile cha uchafuzi alioufanya. Lengo la hii kanuni ni kuhakikisha kuwa mlipaji wa uchafuzi wa mazingira kwanza aogope kuchafua tena mazingira na pili uchafuzi uliofanywa unasawazishwa na ulipajihuo.

Kanuni ya pili ni ile ya **mtuhumiwa wa uchafuaji wa mazingira kuthibitisha mahakanani kuwa hachafui mazingira**. Hii ni kanuni ambayo iko tofauti na sheria nyingine zote ambazo humtaka yule anayemtuhumu mwenzake kuwa amefanya jambo fulani kinyume na sheria fulani kuithibitishia mahakama kuwa kweli mtuhumiwa amefanya vile. Sheria hii ya uhifadhi wa mazingira inatamka wazi kuwa mtuhumiwa wa uchafuzi wa mazingira anatakiwa athibitishe kuwa hachafui mazingira kama inavyodaiwa na mshitaki.

Kanuni ya tatu ni ile **ya ushirikishwaji wa wananchi katika kutathimini athari za kimazingira** katika mradi wowote ule unaotarajiwa kuanzishwa katika eneo fulani. Sheria hii ya uhifadhi wa mazingira inataka ushiriki wa wananchi wa eneo tarajiwa la mradi kuhusishwa moja kwa moja katika hatua zote za kutathimini athari za kimazingira zitakazoletwa na uanzishwaji wa mradi unao tarajiwa kuanzishwa.

Kitu cha msingi cha kukumbuka hapa ni kuwa mradi wowote ule unakatazwa na sheria hii kuanzishwa kabla ya kufanyiwa tathimini ya kina ya athari za kimazingira zitakazotokana na uanzishwaji wa mradi katika eneo Fulani. Ni ukiukwaji wa sheria hii, tena wa makusudi na uliodhahiri kuanzishwa mradi wowote ule nchini Tanzania bila ya ufanywaji wa tathimini ya athari za kimazingira wa kina na wenye ushirikishwaji wa wananchi wa eneo la mradi tarajiwa.

**Kanuni ya uchukuaji wa tahadhari (Precautionary principal)**. Sheria ya uhifadhi wa mazingira imejikita zaidi katika kuhakikisha kuwa uchafuzi wa mazingira hakutokei kabisa na siyo vinginevyo. Msingi mkubwa wa kanuni hii ni kuzuia kuharibika kwa mazingira kwa kufuata msemo wa Kiswahili wa "kinga ni bora kuliko tiba". Hivyo basi sheria hii inachukua tahadhari na kuhakikisha kuwa uchafuzi hautokei kwa kuwa ukishatokea ni vigumu au haiwezekani kabisa kurudisha mazingira katika hali yake ya awali kabla ya uchafuzi huo kufanyika.

**Kanuni ya kuwa juu ya sheria nyingine**. Sheria ya Uhifadhi wa Mazingira ya mwaka 2004, inasema wazi wazi kuwa pindi itakapotokea kuwa sheria yeyote ile inapingana na kipengele chochote cha sheria hii, basi kipengele au vipengele vya sheria ya Uhifadhi wa Mazingira 2004, kitatumika. Katika msingi huu ni wazi kuwa sheria ya mazingira itakuwa juu ya sheria zingine pindi utata utakapojitokeza. Sheria hii inaweka wazi kuwa katika mgongano au utata wowote utakaojitokeza kimaantiki au kitaadhira, basi sheria ya uhifadhi wa Mazingira itumike katika kutoa utata huo. Kimsingi sheria ya uhifadhi wa mazingira ndiyo msingi wa kutatua utata / mgongano huo.

**Haki ya kupata habari za kimazingira:**
Ili mtu aweze kutimiza wajibu wake wa kutunza mazingira, kushiriki kikamilifu katika michakato na maamuzi yanayohusu mazingira ni lazima awe na uhakika wa kupata habari za mazingira ya sehemu na nchi yake, miradi inayofikiriwa kuanzishwa katika sehemu yake na mambo mbalimbali. Haki hii ni haki iliyotiliwa mkazo na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kuwa kila mtu ana haki ya kupata, kutafuta na kupewa habari. Haki hii haina kipingamizi au utofautisho wowote.

Hivyo haishangazi kuona kwamba Sheria ya Mazingira, ya Mwaka 2004 inatambua na kutoa haki kwa kila raia kuwa, anayo haki ya kupewa habari na taarifa zilizoko katika mamlaka za umma zinazohusiana na mazingira, hali ya mazingira, hatari zilizopo na zinazoweza kujitokeza katika mazingira ikiwa ni pamoja na utoaji wa vichafuzi katika maji, hewa au ardhi, utupaji na umwagaji na utunzaji wa takamadhara.

Chapisho hili limeandaliwa kwa lengo la kuwafahamisha wananchi wa Musoma kuhusu hali ya fukwe za ziwa Viktoria katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

**Ni wakati gani ambapo Sheria inadai kuwa haki hii inaweza kutotekelezwa?**

Ombi la taarifa lililotolewa kufuatia maelekezo ya kifungu cha (1) linaweza kukataliwa ikiwa- (a) taarifa inayoombwa itahusisha nyaraka au data ambazo bado hazijakamilika, au mawasiliano ya ndani, au ikiwa ombi hilo linaonyesha wazi halina umuhimu au ni la jumla mno; (b) utulivu na usalama wa taifa utavurugika kutokana na kutolewa kwa taarifa inayoombwa; (c) ni kwa sababu nzuri ya kulinda siri za biashara au viwanda; (d) ombi haliko wazi au halitoi uhakika wa kuwezesha kupambanua taarifa inayoombwa; (e) chombo ambacho ombi hilo limepelekwa kwake, hakina ufahamu wa taarifa inayotafutwa.

Endapo ombi la kupewa taarifa litakataliwa, chombo kilichokataa ombi hilo kitapaswa kutoa sababu za kukataa kwake kwa maandishi.

Inabidi tueleze wazi kuwa ni kosa kwa sheria ya mazingira kutaka kuzuia haki ya wananchi kupata habari eti kwa ajili ya kulinda siri za kiviwanda au kibiashara. Kama habari zinahusiana na mazingira haziwezi kuwa za siri hivyo kwa sharti hilo sheria hii inakiuka kwa uwazi mkubwa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati ni kweli kwamba habari ambazo haziwezi ni zile ambazo zinahatarisha usalama wa taifa, kizuizi hiki hakiwezi kutoa kinga kwa miradi yoyote ile ya kijeshi ambayo inachafua mazingira. Nchi mbalimbali zimetoa uhuru wa wananchi kupata habari za uchafuzi wa mazingira unaofanywa na vyombo vyao vya ulinzi na usalama. Habari ambazo ni siri na haziwezi kutolewa ni zile zinazohusiana na zana za kijeshi, maeneo zinapotunzwa zana hizo au uwezo wa kijeshi wa majeshi ya nchi hiyo. Lakini pale kunapokuwa na uchafuzi wa mazingira katika vyombo hivyo habari hizo lazima ziweze kupatikana.

Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu wao wana haki ya kupata habari zote zinazohusiana na hali ya mazingira ya nchi, vitu vinavyoharibu na kutishia kuharibu mazingira ikiwa ni pamoja na utoaji na umwagaji wa vichafuzi katika maji,

hewa, na ardhi na utupaji na uhifadhi wa takamadhara. Hii ni kuweza kuwawezesha kutenda kazi zao vizuri. Litakuwa ni kosa la jinai kukataa kutoa taarifa iliyoombwa na Mkurugenzi wa Mazingira au Mkurugenzi Mkuu kwa madhumuni ya kutekeleza kazi zinazoendana na madaraka yao kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004.

Ili kuwezesha kuwepo kwa taarifa za mazingira NEMC inatakiwa kukusanya taarifa zinazohusiana na mazingira pamoja na takwimu; kuwa na haki ya kuzipata na kupewa takwimu zozote za mazingira na maliasili; kuchambua taarifa zozote zinazohusiana na mazingira na maliasili; kusambaza habari kwa umma na taasisi binafsi; kufanya tafiti kuhusiana na idadi ya watu na mienendo inayoathiri mazingira na maendeleo; kufanya kampeni za kutoa taarifa na kuelimisha umma juu ya mambo ya mazingira; kubadilishana habari za mazingira na mashirika ya kiraia au taasisi za kikanda na kimataifa; kuratibu usimamizi wa taarifa za mazingira katika wizara za sekta ya mazingira; kumshauri Waziri juu ya mapengo na mahitaji ya taarifa; na mwisho kuanzisha, kwa kushauriana na wizara za sekta ya mazingira, miongozo na taratibu za kukusanya, kuchambua na kusambaza habari na taarifa za mazingira.

Sheria inaitaka NEMC kuanzisha na kuendesha Kitengo cha Habari za Mazingira ambacho kitakusanya na kuweka pamoja ugunduzi na takwimu ambazo zimetolewa na taasisi za umma na binafsi katika harakati zao za kuangalia na kusimamia mazingira. Kwa upande wake Mkrugenzi wa Mazingira anatakiwa kuchapisha ripoti ya hali ya mazingira na usimamizi wa mazingira nchini ambayo inatakiwa kuwasilishwa bungeni. Ni jukumu la wabunge wetu kumdai Mkurugenzi wa Mazingira kuchapisha na kuiwasilisha ripoti hii kwao. Nasi wananchi tunayo haki ya kumdai Mkurugenzi wa Mazingira juu ya uchapishaji wa ripoti hii. Ripoti hii inatakiwa iwe imekamilika na kueleza kwa kinagaubaga hali ya mazingira ya nchi yetu na utendaji wa idara na wizara mbalimbali zinazohusika na sekta ya mazingira. Ripoti hii lazima ieleze mikakati iliyopo

ya kuyalinda na kuyaboreshs mazingira.

Sambamba na jukumu lake la kuchapisha ripoti ya hali ya mazingira Mkurugenzi wa Mazingira anaweza kuchapisha habari yoyote ile anayoiona kuwa ni ya lazima kwa ajili ya elimu ya umma juu ya mazingira na mambo ya mazingira. Hii ni pamoja na kuanzisha mipango na programu zinazolenga kukuza uelewa wa wananchi juu ya maendeleo endelevu na usimamizi wa mazingira. Vilevile Mkurugenzi anatakiwa, kwa kushauriana na wizara za sekta ya mazingira na elimu, kuchukua hatua za kuiingiza masuala ya mazingira katika mitaala ya elimu ya shule, vyuo na taasisi za elimu ya juu.

Baraza la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira nalo lina wajibu wa kufanya upimaji na tafiti kuhusiana na hali ya mazingira na kutoa matarajio au maono yake juu ya mabadiliko ya mazingira kwa upande mmoja na kufanya tafiti ambazo zitachangia katika kuandaa sera na mipangokazi na mikakati inayohusiana na uhifadhi na usimamizi wa mazingira.

Waziri kwa upande wake anaweza kuiteua taasisi yoyote ile kuwa taasisi ya ushauri ya mambo yanayohusiana na ukuzaji wa tafiti-lengwa za kisayansi, utengenezaji wa habari kaitka nyanja ya mazingira, kufuatilia na kupima tija ya vitendo vilivyotendwa.

## 2.2 Sheria Inachosema Kuhusiana Na Fukwe Za Bahari, Maziwa, Mabwawa Na Mito:

Sheria ya Mazingira **Na.20** ya mwaka **2004** inazuia shughuli zilizotajwa katika taarifa hii ikimaanisha uchimbaji mchanga, ujenzi, uchimbaji wa mabwawa ya samaki pamoja na shughuli yoyote ambayo ina asili ya kusababisha uharibifu wa mazingira ya fukwe kufanyika ndani ya mita **60** za eneo la ufukwe:

**Fungu 55** (1): Bila kuathiri masharti yoyote ya sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge, Baraza na mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika na masuala ya mazingira, zitatoa miongozo na kubainisha hatua za kilinda, kingo za mito, mito, maziwa aumiambao ya maziwa na fukwe. (2) Pale ambapo miongozo na hatua zitakapokuwa zimebainishwa kufuatia kifungu cha (1), litakuwa ni kosa kufanya shughuli yoyote kati

ya hizi zifuatazo bila kwanza kupata ruhusa au kibali kilichotolewa na Waziri- (a) kutumia, kusimika, kujenga, kuweka, kubadili, kuongeza, kuondoa, au kubomoa jengo au umbile kwenye au chini ya bahari au fukwe asili za ziwa, ukingo wa mto au bwawa; (b) kufukua, kuchoronga, kutoboa au kuharibu fukwe za bahari au ziwa asili, kingo za mto au kisima cha maji au bwawa; (c) kupandikiza mmea au sehemu yoyote ya mmea, kupandikiza sampuli ya mmea wa kigeni au wa asili uliokufa au ulio hai katika mto unaoingia baharini, kingo za mto au mwambao wa ziwa; (d) kutupa kitu kwenye mto, kingo za mto, ziwa au, ufukwe wa ziwa, ufukwe au ardhi oevu au ndani au chini yake, kiwezacho kuwa na athari mbaya kwa mazingira kwenye mto, kingo za mto, ziwa, fukwe za ziwa au ardhi oevu, (e) kuchepusha au kuzuia mto, ukingo wa mto, ziwa au, mwambao wa ziwa, ufukwe au ardhi oevu kutoka mkondo wake wa asili; (f) kukausha mto au ziwa. (3) Mtu yeyote anayekiuka masharti ya fungu hili anatenda kosa. (4) Waziri anaweza kukasimu madaraka yake chini ya fungu hili kwa Mkurugenzi wa Mazingira, au Ofisa wa mamlaka ya serikali za mitaa au Ofisa kwenye Wizara ya kisekta.

**Fungu 57(1)** inasema, ndani ya **mita sitini** hakutafanyika shughuli yoyote ya binadamu ya kudumu au ambayo kwa asili yake inaweza kuhatarisha au kuathiri vibaya ulinzi wa mazingira na, au utunzaji wa bahari au kingo za mto, bwawa, au miambao ya asili ya ziwa.

**Fungu 73(2)** inasema kuwa pale suala lolote lihusulo usimamizi wa mazingira lifanywapo kwa mujibu wa sheria yoyote iliyopo, linapogongana na sheria hii, Sheria hii (ya mazingira) itatumika.

## 2.3 Adhabu Za Kisheria Kwa Waharifu Wa Mazingira

Adhabu za jumla: **Fungu 191** Adhabu inaanzia sh.50,000 hadi 50,000,000 na kifungo kisichopungua **miezi 3** au kisichozidi **miaka 7** jela au vyote viwili.

**Fungu 188** Makosa yahusuyo **bioanuai:** Faini **million 10** , jela miaka **5** au vyote viwili. Sheria pia inaweka bayana kuwa yeyote aliyesababisha uharibifu atagharimia kurekebisha mazingira yaliyoharibika kwa gharama zake mwenyewe.

Aidha sheria inamtaka mtu aliyesababisha uharibifu wa mazingira katika eneo husika kurekebisha hali hiyo ya uharibifu kwa lengo la kurejesha mazingira hayo sawa au karibia kabisa na hali ilivyokuwa kwenye mazingira kabla uharibifu huo haujatokea. Mkosaji anayepatikana na hatia ya kuharibu mazingira ataamuriwa na mahakama kufanya urejeshaji (restoration) kwa gharama zake mwenyewe.

## 2.4 Hatua Zinazochukuliwa Na Halmashauri Ya Manispaa Ya Musoma Katika Kudhibiti Uharibifu Wa Mazingira

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kupitia kitengo chake cha mazingira inachukua hatua mbalimbali kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa mazingira. Tarehe 24/2/2015 Halmashauri iliitisha kikao cha wadau wa madini ya ujenzi wakiwemo wamiliki na madereva wa malori yanayosafirisha mchanga kwa lengo la kujadili changamoto za upatikanaji wa madini ya ujenzi pasipo kusababisha athari kubwa kwa mazingira. Katika kikao hicho wadau pia walipewa semina kuhusu athari zitokanazo na uchimbaji wa mchanga kwenye fukwe za ziwa na mito. Baada ya somo hilo kueleweka kwa wadau, kwa pamoja walilaani kitendo cha kuchimba mchanga ufukweni hususan ndani ya mita 60 na kuahidi kuacha kitendo hicho.

Maafisa mazingira kwa kushirikiana na Ofisi ya Ukaguzi wa Mji hufanya ukaguzi wa mazingira ya fukwe mara kwa mara kwa lengo la kubaini makosa yanayoweza kufanywa na watu na kusababisha uharibifu wa mazingira kutokea.

Kupitia kaguzi hizo, elimu ya utunzaji wa mazingira imekuwa ikitolewa kwa makundi mbalimbali ya watu wakiwa katika shughuli ambazo Afisa mazingira ataona kuwa zinasababisha au zina uwezekano wa kusababisha athari za kimazingira. Watu hupata fursa ya kupata somo la moja kwa moja.

Afisa mazingira Fikiri Kenyela (mwenye koti) akiwa na wakaguzi wa mji (T.Mayombo na B.R.Maugo) wakitoa elimu ya mazingira kwa wachimba mchanga katika ufukwe wa Makoko.

Wakaguzi wa mji ndg. T.Mayombo (wa kwanza kushoto) na ndg. Bearling R.Maugo wakitoa maelekezo kwa lengo la kudhibiti uharififu wa mazingira ya fukwe.

Halmashauri inafanya operesheni ya kukamata waharibifu wa mazingira kwa kushirikiana na jeshi la polisi na kuwachukulia hatua. Waharibifu wa fukwe wanaokamatwa wakichimba au kupakia mchanga wa ziwani/ufukweni huwekwa rumande (polisi) na kuachiwa baada ya kulipa faini ya Halmashauri ya Manispaa Musoma.

Halmashauri pia iko mbioni kuanza mchakato wa kuziimarisha kamati za mazingira za kata kwa mujibu wa sheria ya Mazingira namba 20 ya 2004, ili ziweze kuwa chachu ya kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika kata zao. Kamati hizo zinatakiwa kujitambua na kujengewa uwezo ili ziweze kuelewa majukumu yao na kufanya kazi iliyokusudiwa kwa mujibu wa sheria.

Halmashauri imeanza mchakato wa kuboresha upatikanaji wa madini ya ujenzi (mawe, moram na mchanga) katika eneo lililotengwa ili kukidhi ongezeko kubwa la shughuli za ujenzi ambazo zinahitaji madini hayo kwa wingi. Hatua hii inachukuliwa ili kuepusha uharibifu wa mazingira unaosababishwa na watu kuchimba mchanga holela hususan ziwani kwenye fukwe. Hili pia ni utekelezaji wa maazimio ya kikao cha wadau kilichotajwa hapo juu. Eneo hilo ni Balima, Mugalanjabo, kata ya Buhare. Tayari

wahandisi wa halmashuri kwa kushirikiana na ofisi ya madini mkoa wa mara na chama cha wachimba madini wadogo (MAREMA), maafisa ardhi na mipango miji wa manispaa wameshakagua eneo na sampuli za madini ya ujenzi kutoka eneo hilo zimepelekwa maabara kwa ajili ya vipimo ili kujua ubora wa madini ya ujenzi kutoka eneo hilo.

Halmashauri pia inao mpango wa kuendelea na zoezi la kutoa elimu kwa umma na wadau mbalimbali wakiwemo waheshimiwa madiwani kuhusiana na masuala yahusuyo utunzaji wa mazingira.

Elimu ya mazingira kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo itatolewa katika kipindi kinachokuja. Aidha mikutano ya hadhara itafanyika kuelimisha wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira. Elimu kwa njia ya redio, majarida na vipeperushi ni mbinu nyingine nzuri kwa ajili ya kuelimisha jamii juu ya utunzaji mazingira.

## 3.0 Changamoto Zinazokwamisha Utunzaji Na Uhifadhi Wa Mazingira Katika Halmashauri Ya Manispaa Ya Musoma

Zipo changamoto zinazorudisha nyuma juhudi za kuhifadhi na kutunza mazingira ya fukwe za ziwa viktoria kama ifuatavyo;

1. Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sababu za kisayansi za kuhifadhi ufukwe wa ziwa, mito, mabwawa na bahari
2. Baadhi ya watu kukaidi maagizo ya kamati za mazingira
3. Shughuli za ujenzi wa maabara ndani ya manispaa ya Musoma kuwekewa sharti la kujengwa kwa kutumia mchanga wa ziwani pekee. Hii kwa yenyewe ni uharibifu wa mazingira lakini pia imezorotesha operesheni ya kukamata waharibifu wa mazingira.
4. Kuwepo kwa vikundi vya watu wanaopakia mchanga wa ziwani wakati wa usiku ili wasiweze kutambulika kirahisi na kuchuliwa hatua
5. Wanaojenga nyumba ndani ya mita 60 wanadai kuwa walimilikishwa viwanja hivyo na halmashauri. Aidha wanadai kuwa ziwa ndilo limewafuata na kuvamia viwanja vyao na kujikuta wako ndani ya mita 60 hususan baada ya mvua za El-nino.
6. Mtizamo wa wengi kuwa mchanga wa ziwani ndio mchanga wenye ubora zaidi na ndio pekee unaofaa kwa ujenzi.

7. Watu wengi kuanzisha mabwawa ya kufugia samaki kando kando ya ziwa ili kuwa na chanzo cha uhakika cha maji. Aidha mtizamo wa wadau wa sekta ya uvuvi ni kuwa mabwawa yanayochimbwa kandokando ya ziwa hayana athari kwa ziwa na yanasaidia kupunguza kuisha kwa samaki kwa kasi ndani ya ziwa. Mitizamo hii inachochea zana ya uchimbaji wa mabwawa ya kufugia samaki ndani ya mita 60 na kusababisha uharibifu wa fukwe.

8. Ukosefu mkubwa wa bajeti ya mazingira katika halmashauri ya manispaa ya Musoma.
9. Halmashauri zingine ndani ya mkoa wa Mara kutoa vibali kwa watu kununua au kuchimba na kusafirisha mchanga wa ziwani. Hili limeshuhudiwa katika halmashauri ya Butiama. Mchanga ulionunuliwa Musoma vijijini (Mumahare) unaingizwa ndani ya halmashauri ya Manispaa ya Musoma.

Uchimbaji wa mchanga Mmahale, Musoma vijijini (Wilaya ya Butiama)

## 3.1 Utatuzi wa Changamoto

1. Elimu ya mazingira inahitajika sana kutolewa kwa jamii nzima ili kukuza uelewa wao wa masuala ya mazingira sanjali na kuelewa umuhimu wa kulinda mazingira. Elimu hii ya mazingira ni vyema ikaanza kutolewa katika ngazi ya chekechea hadi elimu ya juu. Somo maalumu linalojitegemea liongezwe katika mtaala wa shule za msingi na sekondari na katika ngazi ya elimu ya juu na vyuo vinginevyo, somo la mazingira liwe ni lazima mwanafunzi kulifaulu ili apate sifa ya kuhitimu ngazi husika ya masomo au kuendelea ngazi inayofuata. Katika ngazi zote uangalifu mkubwa utumike kuhakikisha kuwa mada za msingi hususan zinazokuza uadilifu wa watu katika kuyatunza mazingira yao kwa manufaa ya kizazi kilichopo leo na vile vitakavyofuata. Aidha, viongozi wa dini wananafasi kubwa ya kuhimiza kampeni ya utunzaji mazingira kwa kutoa elimu kwa waumini wao kuhusu kuyatunza mazingira kama Mungu alivyowaagiza Adamu na Hawa

   kuilima na kuitunza bustani ya Edeni (Mwanzo 2:15). Mungu amemweka mwanadamu kuwa mlinzi wa mazingira kwa manufaa ya viumbe wengine wote. Siku zote yeye (Mungu) anatamani tuishi katika mazingira safi na salama yenye

kutupatia mahitaji yetu yote ya msingi, ndiyo maana amepanga kuturudishia Paradiso iliyopotea (nchi mpya)(Isaya 65:17). Wanasiasa, watawala, wasomi na watu mashuhuri kwa vile wana nafasi kubwa ya kusikilizwa kwa heshima kubwa waliyonayo katika jamii wanatakiwa kufanya masuala ya utunzaji wa mazingira na kukemea uharibifu wa mazingira kuwa agenda yao ya kudumu.

2. Serikali inatakiwa kutenga bajeti ya kutosha katika kampeni ya kuhimiza utunzaji wa mazingira mathalani upandaji miti, uzoaji na utupaji wa taka ngumu na maji taka, elimu ya mazingira kwa jamii. Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inatakiwa kuyapa upendeleo mambo yanayopelekea mazingira kutunzwa.

3. Usimamizi wa sheria ya mazingira namba 20 ya mwaka 2004, kanuni zake pamoja na sheria zingine zinazohimiza kulinda mazingira ni budi kuwekewa mkazo mkubwa. Kwa vile watu wengi hukaidi makusudi utaratibu wa sheria, ni muhimu sana usimamizi wa kina ufanywe na ofisi kuu ya mkurugenzi kwa kutumia idara yake ya mazingira na kushirikisha wadau wengine likiwemo jeshi la polisi. Watu wanaojihusisha na uharibifu wa mazingira wachukuliwe hatua za kisheria mara moja ili kuwa fundisho kwa wengine.

4. Idara zingine za serikali, mashirika ya umma na sekta binafsi hawana budi kuzingatia sheria ya mazingira katika kutekeleza miradi yao mbalimbali na utendaji wa siku kwa siku. Mathalani ugawaji wa viwanja unaofanywa na idara ya ardhi kwa ajili ya makazi au shughuli yoyote ya binadamu isiyoruhusiwa kufanyika ndani ya mita 60 za ziwa ni vyema ukasitishwa mara moja ili kulinda mazingira yetu kwa faida ya wote.

5. Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ni vyema ikatenga eneo maalumu kwa ajili ya kuchimba madini ya ujenzi hususan mchanga, mawe na changarawe. Uchimbaji wa madini hayo kwenye fukwe au eneo jingine lisiloruhusiwa usitishwe mara moja.

6. Tathmini ya athari kwa mazingira na kijamii (ESIA) kwa mujibu wa sheria kuhusu miradi iliyoainishwa na sheria ifanyike kwanza na baada ya kibali kutolewa ndipo utekelezaji uanze.

7. Vikundi vya kutunza mazingira ya fukwe (BMU) vijengewe uwezo wa kusimamia mazingira ya fukwe. Elimu itolewe kwa vikundi hivi ili visaidie kusimamia fukwe za ziwa.

8. Jamii ijenge utamaduni wa kukemea uharibifu wa mazingira na kuwataja waharifu wanaojihusisha na uharibifu wa mazingira mathalani uvuvi wa kutumia sumu, uchimbaji wa mchanga ufukweni na kilimo ndani ya mita 60.

9. Upandaji miti unahitajika sana kupewa kipaumbele ili kulinda vyanzo vya maji zikiwemo fukwe za ziwa.

## 4.0 Majukumu Ya Mamlaka Za Serikali Za Mitaa Katika Kusimamia Uhifadhi Wa Mazingira

Sheria ya Mazingira Na.20 ya mwaka 2004 (EMA) inaweka bayana wajibu wa serikali za mitaa katika suala zima la kusimamia uhifadhi na utunzaji wa mazingira. **Fungu la 36**
(1) Kila Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Wilaya na Mji itateua au kuajiri Ofisa Usimamizi wa Mazingira ambaye atakuwa Ofisa wa umma na atakuwa;
(a) kwenye eneo la mamlaka ya Jiji, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Jiji;
(b) kwenye eneo la mamlaka ya Manispaa, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Manispaa;
(c) kwenye eneo la mamlaka ya Wilaya, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Wilaya; na
(d) kwenye eneo la mamlaka ya Mji, Ofisa Usimamizi wa Mazingira atajulikana kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Mji.

**Kifungu cha (2)** kinasema; Mtu aliyeteuliwa au kuajiriwa na Halmashauri ya Jiji, Manispaa, Wilaya au Mji kama Ofisa Usimamizi wa Mazingira atakuwa mwenye shahada au stashahada kutoka asasi ya elimu ya juu inayotambulika na mwenye uwezo katika usimamizi wa mazingira

**Kifungu cha (3)** Ofisa Usimamizi wa Mazingira atakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) kuhakikisha utekelezaji wa Sheria hii kwenye eneo lake la kazi;
(b) kushauri Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya eneo lake la kazi kuhusu masuala yote ya mazingira;
(c) kukuza weledi kuhusu ulinzi wa mazingira na uhifadhi maliasili kwenye eneo lake;
(d) kukusanya na kusimamia taarifa kuhusu mazingira na matumizi ya maliasili kwenye eneo hilo;
(e) kuandaa taarifa za mihula kuhusu hali ya mazingira ndani ya eneo husika;
(f) kufuatilia maandalizi, mapitio na vibali vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA) kwa ajili ya uwekezaji wa ndani;
(g) kufanya mapitio ya sheria ndogo zinazohusu usimamizi wa mazingira na shughuli maalumu za kisekta zinazohusiana na mazingira;
(h) kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu kuhusu utekelezaji wa Sheria; na
(i) kutekeleza majukumu mengine kwa kadiri mamlaka ya serikali za mitaa itakavyokuwa ikiyatoa.

## 4.1 Kamati Za Kudumu Za Mamlaka Za Serikali Za Mitaa

Fungu la 37 (1) Kamati ya Kudumu ya Mipango Miji na Mazingira iliyoanzishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 42 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ya mwaka 1982, pamoja na Kamati ya Kudumu ya Masuala ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira

iliyoazishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 74 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982, kila moja itakuwa Kamati ya Usimamizi wa mazingira ya Jiji, Manispaa au Wilaya kuhusiana na Jiji, Manispaa, na Wilaya kwa kila moja ya Kamati ya Kudumu iliyoanzishwa.

(2) Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya Jiji, Manispaa na Wilaya itatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa chini ya vifungu vya (1) na (2) vya fungu la 55 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ya mwaka 1982 na kama itakavyokuwa, vifungu vya (1) na (2) vyafungu la 118 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982 pamoja na kanuni zilizotengenezwa chini ya sheria hizo. (3) Bila kuathiri kifungu cha (2), Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya Jiji, Manispaa na Wilaya pia- (a) itatekeleza kazi nyingine za ziada kama zilivyobainishwa na Sheria hii au kama, kwa nyakati mbalimbali, itakavyoagizwa na Waziri kwa Jiji, Manispaa au Wilaya kupitia taarifa iliyotangazwa kwenye *Gazeti la Serikali*; na (b) kutekeleza maagizo yoyote yaliyotolewa kwao na Waziri yanayohusu kuendeleza na kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira.

## 4.2 Kamati za Kudumu za Miji, Kata, Vijiji na Vitongoji

**Fungu 38** (1) Kila Kamati ya Kudumu ya Masuala ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ya mji iliyoanzishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 96 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982, kamati maalumu iliyoundwa kufuatana na fungu la 107 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982 pamoja na Kamati ya Maendeleo ya Kata iliyoanzishwa chini ya kifungu cha (1) cha fungu la 31 la Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982,yanayohusu eneo ilimoanzishwa Kamati hiyo- (a) itawajibika kusimamia mazingira kikamilifu yanayohusu eneo ilimoanzishwa; (b) itatekeleza kazi nyingine za ziada kama zilivyobainishwa na Sheria hii au kama itakavyoagizwa na Waziri au Baraza, kwa kila mmoja au mmojawapo; (c) itatekeleza maagizo yote yatakayotolewa kwake na Waziri yanayohusu kuendeleza na kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira; na (d) itatekeleza majukumu au kazi zingine zozote zinazohusiana na usimamizi unaofaa kwa mazingira kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982.

(2) Kamati ya Maendeleo ya Kijiji ya kila kijiji itawajibika kusimamia kikamilifu mazingira kwenye eneo ilimoanzishwa na kwa utaratibu huo inaweza kufanya majukumu mengine yaliyotolewa chini ya ibara (a), (b), (c) na (d) za kifungu cha (1).

### 4.3 Uteuzi wa Ofisa Usimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji

**Fungu la 39** linasema: Halmashauri ya Wilaya itamteua Ofisa wa umma kwa ajili ya kila eneo la utawala la mji, kata, kijiji, Mtaa na Kitongoji ambaye-
(a) kwenye eneo la mamlaka ya mji ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Mji;
(b) kwenye eneo la mamlaka ya Kitongoji ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Kitongoji;
(c) kwenye eneo la mamlaka ya Kata ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Kata;
(d) kwenye eneo la mamlaka ya Mtaa ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Mtaa; na
(e) kwenye eneo la mamlaka ya Kijiji ataitwa Ofisa Usimamizi Mazingira wa Kijiji.

### 4.4 Kazi za Ofisa Msimamizi wa Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji.

Fungu la 40 linaweka bayana kazi za Ofisa Usimamizi Mazingira wa Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji itakuwa ni kuratibu kazi zote na shughuli zinazolenga kuhifadhi mazingira kwenye eneo la mji, kata, mtaa, kijiji na kitongoji, au kadiri itakavyokuwa ndani ya Wilaya ya eneo husika.

### 4.5 Madaraka ya jumla ya Kamati za Usimamizi wa Mazingira za Jiji, Manispaa, Wilaya, Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji:

Kila Kamati ya Usimamizi wa Mazingira inayohusu eneo ilimoanzishwa, itakuwa na madaraka ya;
(a) kuanzisha uchunguzi na upelelezi kuhusu tuhuma yoyote inayohusu mazingira na utekelezaji au ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii;
(b) kumtaka mtu yeyote kutoa maelezo au taarifa kuhusu suala lolote linalohusu mazingira;
(c) kutatua migogoro kati ya watu binafsi, makampuni, wakala, asasi zisizokuwa za kiserikali, idara au asasi za Serikali, inayohusu majukumu, kazi, uwezo, wajibu au shughuli zao chini ya Sheria hii;
(d) kukagua na kuchunguza makazi, mtaa, gari, ndege au sehemu nyingine yoyote au kitu kinachoaminika au kuna sababu za msingi kuamini kuwa kichafuzi au vitu vingine vinavyoaminika kuwa vichafuzi vimewekwa au vinasafirishwa;

(e) kumtaka mtu yeyote aondoe kwa gharama yake, kitu au dutu yoyote kutoka mahali popote panapoaminika kuwa kitu au dutu hiyo inaweza kuhifadhiwa kwa usalama au kuharibiwa bila kuleta madhara kwa afya; na

(f) kufungua kesi za madai au jinai dhidi ya mtu yeyote, kampuni, wakala, idara au asasi inayoshindwaau kukataa kufuata agizo lolote lililotolewa na Kamati hizo.

## 5.0 Hitimisho

Ni vyema kulinda mazingira yetu pasipo kusubiri mkondo wa sheria kuchukua nafasi yake kwani mazingira bora ni kwa faida yetu wenyewe na vizazi vijavyo. Madhara ya kuharibu mazingira ni makubwa kuliko faida kwa sababu yanaathiri binadamu na viumbe wengine wanaoishi sasa na vizazi vijavyo. Ni muhimu kwa watu wote kulinda fukwe za ziwa letu. Shughuli yoyote yenye kusababisha uharibifu wa fukwe kama ilivyoelezewa katika makala hii ni vyema ifanyike nje ya mita 60 zilizotengwa kwa mujibu wa sheria. Madini ya ujenzi tuyapate kutoka katika maeneo rasmi yaliyotengwa na halmashauri kwa lengo hilo.

Kama tutaruhusu kila eneo kuchimbwa madini ya ujenzi kama kila mtu atakavyojisikia, basi athari zake ni kubwa kimazingira ambazo ni pamoja na kuharibu ubora wa viwanja, kusababisha mashimo kila mahali yanayoweza kusababisha ajali, kuharibu mwonekano wa mji na kuongeza gharama za kuendeleza viwanja vilivyoharibika. Suala la kuzuia uharibifu wa mazingira ni suala nyeti. Jukumu la kulinda na kuhifadhi mazingira ni letu sote.

Imeandaliwa na:

FIKIRI KENYELA
**AFISA MAZINGIRA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA**